

### Kuwahudumia Wengine katika Imani

Rais Uchtdorf anatuambia sisi kwamba imani yetu kwa Mungu *lazima* "iambatane na matendo." Wakati imani yetu "imefungwa nira pamoja na tendo endelevu," anaelezea, "huijaza . . . nafsi kwa amani na upendo." Pamoja na ahadi ya baraka hii, sisi *tunaweza* kuleta tofauti, na *tunaweza* kuona hili katika maisha yetu kama tunachukua muda wetu kufanya huduma iliyojaa-imani. Unaweza kuomba kila asubuhi ili kumwomba Bwana msaada katika kuwatumikia wengine. Kwa mfano, muombe Yeyeakuonyeshe wakati ndugu zako wanahitaji msaada wa kazi ndogo ndogo au wakati rafiki anahitaji kupongezwa. Kisha, wakati unapopokea msukumo utendee kazi! Kama ukiyafanya maombi na huduma hii kuwa tabia, ndipo, matendo yako ya uaminifu na endelevu yatabariki maisha yako na maisha ya wengine. Rais Uchtdorf ameahidi kwamba wewe "unaweza kuwababilisha watu, familia, mataifa, na ulimwengu."



## WATOTO

### Amini

Jaribu shughuli hii pamoja na rafiki. Unatakiwa kuamini na kufuata mwongozo wao kwa uangalifu.

Kwa kalamu au penseli katika mkono wako, fumba macho yako. Acha rafiki yako akuambie wapi kwa kuchora macho, pua, mdomo, na nywele katika sura hii. Kisha angalia. Inaonekana namna gani? Unaweza kupaka rangi usoni na kuchora nyingine ili kucheza tena!

Wakati mwingine ni vigumu kufuata maelekezo. Lakini wakati tunapojaribu kumfuata Baba wa Mbinguni kwa kumsikilia-za Roho Mtakatifu, Yeye atatusaidia. Tunaweza daima kumwamini Yeye.

